

**TAARIFA FUPI YA MRADI WA UJENZI WA BWENI LA WASICHANA KIDATO CHA TANO NA SITA  
KATIKA SHULE YA SEKONDARI MISUNGWI TAREHE 15/09/2020.**

**1.0 UTANGULIZI**

Shule ya Sekondari Misungwi ni shule pekee ya Serikali katika Wilaya ya Misungwi yenye kidato cha tano na cha sita na ndio shule pekee yenye Bweni 1 la wasichana lenye uwezo wa kubeba wanafunzi **48** kutokana na idadi kubwa ya wanafunzi kuongezeka na kusababisha upungufu wa miundombinu ya bweni la kuweza kukidhi mahitaji ya wanafunzi.

Shule imeanzisha Mradi wa Ujenzi wa Bweni jipya la wanafunzi wa kidato cha tano na cha sita lenye uwezo wa kulala **wanafunzi 80** ambapo jengo hili lina vyumba 4 vya kuogea, vyoo vyumba 4 na sehemu ya kuanika nguo.

**2.0 GHARAMA YA MRADI**

Gharama ya mradi huu inakadiriwa kutumia kiasi cha **Tshs 111,691,750/=** kukamilisha ujenzi wa jengo pamoja na Samani zake na ujenzi ulianza mwaka wa fedha 2018/2019.

**3.0 HATUA YA MRADI.**

Mradi huu upo hatua ya ukamilishaji ambayo ni asilimia 75 ya ujenzi ambapo kwa sasa tayari Jengo limeezekwa na kupigwa lipu na mashimo ya choo yanaendelea kuchimbwa, maandalizi ya kuweka vigae, bodi pamoja na kupaka Rangi ndani na nje, kuweka miundombinu ya umeme na maji, Fedha iliyotumika hadi sasa ni **Tsh. 66,728,859/=** ikiwa ni gharama za kujenga boma, kuuzeka, kupiga lipu na manunuzi ya vifaa na ufundi.

**4.0 VYANZO VYA FEDHA YA MRADI NI.**

1. Kubana matumizi ya fedha za chakula Kununua chakula kwa bei ya sokoni 35,000,000/=
2. Kubana matumizi ya Pesa ya ada Tshs. 9,000,000/= (Wanafunzi wa A'Level).
3. Ahadi ya Mhe, Professa Joyce Ndalichako **(MB)** Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. ahadi hiyo aliitoa tarehe 09/11/2019 ya tshs. 31,000,000 pamoja na Samani zake ikiwa ni Vitanda 40 pamoja na "Locker" yenye thamani Tsh. 17,360,000/= katika ziara yake.

Nawasilisha,

Anna Urio  
Afisa Mipango (W)  
**MISUNGWI**

**PICHA HAPA CHINI, IKIONYESHA MAENDELEO YA MRADI WA UJENZI WA JENGO LA BWENI LA WASICHANA KATIKA SEKONDARI KWA HATUA YA UKAMILISHAJI**



**PICHA HII, IKIONYESHA MWONEKANO NA NAMNA UJENZI WA VYUMBA VYA KULALA WASICHANA WA SHULE YA SEKONDARI YA MISUNGWI PAMOJA NA UWEKAJI WA DARI JUU UKIENDELEA.**

